

HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

SHULE YA SEKONDARI ITUNDURU
S.L.P 137,
IGUNGA.

08/12/2020

JINA LA MWANAFUNZI

SHULE ATOKAYO

S.L.P

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahikukuarifu kwamba umechaguliwa kujiuna na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.
HONGERA SANA.

Mhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021** siku ya jumatatu saa 1:00 Asubuhi bila kukosa.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 Wasichana (Sare za Shule)

- (i). Sketi ya Light blue nzito yenye marinda ya kupanga na urefu wa kupita magoti jozi (pair) mbili.
- (ii). Mashati mawili tetroni mikono mifupi (Mzazi ashone mwenyewe).
- (iii). Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na urembo wala visigino virefu vyenye kupigwa brush (vya kamba).
- (iv). Soksi ndefu nyeupe (stockings) jozi mbili sentimita 15 zisizo na urembo wowote.
- (v). Wasichana wa madhehebu ya kiislamu wanaopenda HIJAB wanaruhusiwa na iwe na rangi ya uniform.
- (vi). Sweta la rangi ya light blue la kuvaa wakati wa baridi
- (vii). T-shirt mbili rangi yakijani .
- (viii). Dictionary na kamusi kwa matumizi yake binafsi.
- (ix). Sketi nyeusi nzito kwaajili ya kazi za nje.
- (x). Viatu vya michezo rangi yoyote.
- (xi). Daftari 10 kubwa aina ya (**Counter Book 2Q**).
- (xii). **Daftari ndogo hazihitajiki**

2.2. Wavulana

- (i). Suruali ya light blue nzito yenye mashono ya kawaida jozi mbili mifuko ya pembeni (usishone pisto)
- (ii). Mashati mawili tetroni mikono mifupi (Mzazi anunue mwenyewe).
- (iii). Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na urembo wala visigino virefu vyenye kupigwa brush (Vya kamba)
- (iv). Soksi ndefu nyeusi (stockings) jozi mbili sentimita 15 zisizo na urembo wowote
- (v). Viatu vya urembo rangi yoyote.
- (vi). Sweta la light blue la kuvaa wakati wa baridi.
- (vii). T-shirt mbili rangi ya light blue.
- (viii). Mkanda wa ngozi rangi nyeusi
- (ix). Daftari 10 aina ya (**Counter Book 2Q**) na vifaa vya jometri (set au kasha)
- (x). Dictionary na kamusi kwa matumzi yake binafsi.
- (xi). Suruali nyeusi kwa ajili ya kazi za nje.
- (xii). Track suti ya kijani iliyokolea kwa ajili ya michezo (suruali tu).
- (xiii). **Daftari ndogo hazihitajiki.**

2.3. VIFAA VINGINE KWA UJUMLA.

- (i). Mfagio wa nje (Hard Broom)
- (ii). Faili folder moja

ANETH ROBERT
MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA
SHULE YA SEKONDARI ITUNDURU

FOMU YA MZAZI/MLEZI YA KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA,
KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YA SHULE

Mimi(taja majina yako matatu)
Mzazi/ mlezi wa Kidato cha kwanza
2019(Taja jina la mwanafunzi).

Kitongoji cha Kijiji cha kata
ya Tarafa ya wilaya ya
mkoa wa

Nakiri kuwa nimesoma kwa makini na kuelewa sheria zote za shule, kanuni, maelekezo
na maagizo mbalimbali ya shule na kuahidi kuyatekeleza kikamilifu.

.....
(Sahihi ya mzazi/Mlezi)

Namba ya simu

SEHEMU B-MWANAFUNZI

Mimi wa shule ya
msingi ninakubali kujiunga na shule ya sekondari Itunduru na
nitafuata masharti yote na sheria za shule zote.

SAINI.....

TAREHE

.....
(jina na sahihi ya mkuu wa shule)

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

ITUNDURU SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 137, IGUNGA.

Date.....

Ref.No.....

The Medical Officer (Government Hospital)

.....
.....

PART A:REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

Mr/Mrs/Miss..... (Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time secondary education .The examination should include the following ineligible incase of a defect. Pregnancy (Category 4) will also render a girl ineligible for a secondary education.

1.(a)Eye sight(b)speech(c)Hearing(d)Limb(e)Venereal Deceases (f)Leprosy (g)Epilepsy.

PART B:MEDICAL CERTIFICATE

(a)Eye sight.....

(b)Hearing.....

(c)Speech.....

(d)Limb

(e)Venereal Deceases.....

(f)Leprosy.....

(g)Epilepsy.....

2. Neuroses

3. Other serious deceases.....

4. Pregnancy.....

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for a full –time secondary education.

Designation.....Date.....

Signature &Official Stamp

To be completed by a government Officer)

NB: Incase of any serious health problem(s), the records from the Government Hospital must be submitted to school while reporting.

3.0 SHERIA ZA SHULE

Ni marufuku mwanafunzi kufanya yafuatayo:-

- (i). Kutoka nje ya shule kabla ya mda wa kuruhusiwa bila kibali.
- (ii). Kuzurula nje wakati wa vipindi.
- (iii). Kuwa na simu shuleni.
- (iv). Kufuga ndevu, nywele, kucha, kupaka rangi na kusuka nywele.
- (v). Kuingia bila ruhusa sehemu zifuatazo;.Ofisi za walimu,maabara,jikoni,Hosteli na nyumba za wafanyakazi.
- (vi). Kutembelea vilabu vya pombe , kumbi za starehe kwenye sehemu za kucheza kamali na nyumba za kulala wageni.
- (vii). Kukimbia mitihani na majaribio.

3.1 MWANAFUNZI ATAFUKUZWA SHULE KAMA ATAFANYA MAKOSA YAFUATAYO:-

- (i). Kusababisha au kupata mimba.
- (ii). Kupiga au kupigana
- (iii). Kutoroka shuleni
- (iv). Kugoma kufanya adhabu AU Kumpiga mwalimu
- (v). Kujihusisha na wizi
- (vi). Kukutwa na simu shuleni
- (vii). Kuhamasisha migomo.
- (viii). Kushiriki matendo ya uhalifu.
- (ix). Kujihusisha na mapenzi ndani na nje ya shule.
- (x). Kutumia kilevi cha aina yoyote.
- (xi). Kudharau wimbo au bendera ya taifa.
- (xii). Kuoa au kuolewa
- (xiii). Uasherati na ushoga